

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA AWALI NA MAFUNZO YA UFUNDI
KIFURUSHI CHA LIKIZO MWEZI WA NNE -2020
KISWAHILI VI

JINA: _____ TAREHE: _____

MUDA 1.30

SEHEMU A: SARUFI

Chagua jibu sahihi na ujaze kwenye boksi herufi ya jibu

1. Neno lipi linakamilisha sentensi “tulitembea kwa miguu ____ sokoni.
(a) Hata (c) Mpaka
(b) Kabisa (d) Sasa
2. Wale wanakwenda wapi? Katika sentensi neno “wale” limetumika kama aina gani ya maneno?
(a) Kitenzi (c) Kitenzi
(b) Kiwakilishi (d) Nomino
3. Baraka hupenda kusoma. Sentensi hiyo iko katika hali ipi ya vitenzi?
(a) Mazoea (c) Kuendelea
(b) Ijayo (d) Ya sasa
4. Kaka anacheza na dada anapika. Katika aina za sentensi hii ni aina gani?
(a) Shurutia (c) Ambatano
(b) Tegemezi (d) Changamano
5. “Kiatu kimepotea” sentensi hii ipo katika ngeli ipi?
(a) I-ZI (c) U-ZI
(b) A-WA (d) KI-VI
6. Du! Alipigwa mpaka basi. Neno Du! Limesimama kama
(a) Kitenzi (c) Nomino
(b) Kihisishi (d) Kielezi
7. Neno kompyuta kwa jina lingine huitwa_____
(a) Mpakato (c) Tarakilishi
(b) Simu ya mkononi (d) Tochi
8. Mtoto aliyejuja ameondoka neno lililopigwa mstari ni aina gani ya kiambishi awali;
(a) Rejeshi (c) Tamati
(b) Nafsi (d) Kionyeshi
9. Neno “Mwaga” katika kauli tendeka litakuwa;—
(a) Mwagwa (c) Mwagana
(b) Mwagika (d) Mwagia
10. Ni kitabu chenye orodha ya maneno yaliyopagwa kwa alfabeti huitwa;
(a) Kamusi (c) Orodha
(b) Risala (d) Rejea
11. Risala imegawanyika katika sehemu kuu ngapi?
(a) Tatu (c) Sita
(b) Nne (d) Saba
12. Ni umbo la neno linalobeba maana ya msingi ya neno
(a) Msingi (c) Nomino
(b) Mzizi (d) Neno

13. "Anasoma" katika neno hilo ipi ni mzizi wa neno?
 (a) A (c) Som
 (b) An (d) Ma
14. Viambishi vinavyopachikwa kabla ya mzizi huitwa;-
 (a) Viambishi kati (c) Viambishi tamati
 (b) Viambishi awali (d) Viambishi rejeshi
15. "Fedha anaimba vizuri" sentensi hii ipo katika njeo gani?
 (a) Iliyopita (c) Unaopita
 (b) Uliopo (d) Ujao
16. "Juma alinipita" kiambishi kiwakilishi ni?
 (a) Li (c) Ta
 (b) Ma (d) Ni
17. Kipande cha neno ambacho hupachikwa kwenye mzizi wa neno
 (a) Mzizi (c) Msingi
 (b) Kiambishi (d) Tamati
18. Habari iliyofupishwa huitwa_____
 (a) Habari fupi (c) Sentensi
 (b) Hotuba (d) Muhtasari
19. Taarifa ya wazi kwenye chombo cha habari
 (a) Shairi (c) Tangazo
 (b) Taarifa ya habari (d) Gazeti
20. Mstari wa mwisho katika ubeti usiobadilika
 (a) Kibwagizo (c) Kituo kimalizio
 (b) Kituo bahari (d) Nusu bahari

SEHEMU B: LUGHA YA KIFASIHI

21. Kamilisha methali, _____ hawachi kuonana.
 (a) Wapendanaao (c) Wema
 (b) Walio hai (d) Mahasidi
22. Ni nahau ipi yenyе maana juta au sikitika
 (a) Tia ndani (c) Uma kidole
 (b) Vuta Subira (d) Shika usukani
23. Kama unakipenda kwa nini usikile? Jibu la kitendawili hiki ni
 (a) Ulimi (c) Tumbo
 (b) Macho (d) Miguu
24. Jibu la kitendawili "Nikivaa nguo sipendezi, nikivua napendeza ni
 (a) Nyanya (c) Pilipili
 (b) Kitunguu (d) Karoti
25. "Maisha" ni jibu la kitendawili kipi?
 (a) Ugumu wa Maisha (c) Ajenga ingawa hana mikono
 (b) Nina kijiti changu nizidivyo (d) Wana wa mfalme wepesi kujifisha
 kukata ndivyo

SEHEMU C; jaza kwa kuchagua jibu kwenye sanduku

26. _____ ni neno linaloeleza tendo lilivyofanywa, litakavywa fanywa na mtenda.
27. _____ ni maneno ambayo yanaunganishwa kwa herufi za kwanza
28. _____ ni tungo fupi za kisanaa ambazo hutoa wosia au nasaha kwa lugha ya mafumbo
29. _____ ni hoja zilizojadiliwa kwenye mkutano
30. _____ ni kifungu cha maandishi kilichoandikwa kutokana na mtazamo wa mwandishi ili kujadili mada Fulani.

TOA MAANA YA MANENO YAFUATAYO

31. Uzalendo
32. Sentensi
33. Tarakilishi
34. Viambishi tamati
35. Muwala

SEHEMUD: USHAIRI

Soma shairi lifuatalo na kisha ujibu maswali
 Mashairi mashuhuri, pamoja na wanachuo,
 Hodari kwa kufikiri, kufunga yenye matao,
 Ilipofika safari, kwenda kusiko rejea,
 Hawakuwa na saburi, wote wamekwenda zao.

Walikuwa wapendezi, wakifadhili wenzao,
 Wakapendwa kwa wapenzi, ajabu mfano wao,
 Kurejea hawawezi, japo tulie vili,
 Kwa kilio na machozi, hawarudi watu hao.

Walitenda ya hekima, katika uhai wao,
 Wakawa wenye huruma, kwa sifa zao nav yeo,
 Kwa hali ya taadhima, sifa zikenda mpeo,
 Wote hao umezama, zimebaki sifa zao.

36. Shairi hili lina beti ngapi? _____
37. Vina vya kati na mwisho vya ubeti wa pili ni _____
38. Mtunzi wa shairi anaposema' ilipofika safari "maana gani? _____
39. Ni aina gani ya kituo katika shairi hili? _____
40. Shairi ulilosoma ni aina gani ya shairi? _____

Andika sehemu kuu tano za muundo wa uandishi wa kumbukumbu kwa kufuata utaratibu

41. _____
42. _____
43. _____
44. _____
45. _____

SEHEMU E: UTUNGAJI

Sentensi zifuatazo haziko katika mfululizo ufaao. Zipange ziwe katika mfululizo ufaao kwa kuandika herufi A,B,C,D na E

46. Walifurika katika viwanja vya shule ya msingi furaha
47. Ili kuwa ni siku ya jumamosi
48. Watu wengi hawakwenda kazini siku hiyo
49. Hata wanafunzi walikuwa na furaha sana siku hiyo
50. Siku ya sherehe iliwadia